



Mratibu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Remmy Lema, akielezea jambo kuhusu mradi, katikati ni Mratibu msaidizi na Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa MJUMITA Mama Leneth Motto.

Wanamitandao kanda ya Nyanda za juu Kusini waupokea mradi wa haki katika misitu kwa shangwe.

Na Remmy Nsua- Mratibu wa Kanda

Mradi wa haki katika misitu wenye lengo la kuhakikisha kuwa huduma zitokanazo na mfumo ikolojia wa misitu zinahifadhiwa kwa manufaa ya jamii na taifa kwa kuona kwamba faida zitokanazo na mfumo huo zinafaidisha wanajamii wote waishio pembezoni mwa misitu umepokelewa kwa furaha kubwa na wanajamii wa Iringa. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na unafadhiliwa na mfuko wa AcT (Accountability in Tanzania). Katika kanda ya nyanda za juu kusini mradi huu umeanza kutekelezwa katika mkoa wa Iringa katika wilaya zake tatu ambazo ni Iringa Vijijini, Mufindi na Kilolo. Katika kanda ya nyanda za juu kusini tuna mitandao tisa ambayo ni New dabaga Ulongambi, Idete, Udekwa na Kising'a lugalo (Kilolo)

Kitapilimwa, Nyang'oro kusini na Nyang'oro kaskazini (Iringa Vijijini) Msaluki na Ilondo (Mufindi).

Mradi huu una mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba lengo linatimia. Mikakati hiyo ni kama ufuatiliaji utawala wa misitu na hali ya misitu, tafiti, chambuzi na mawasiliano, matumizi ya viwango vya kimataifa na kuhamasisha utekelezaji wa sheria za misitu. Baada ya kuelezwa mikakati hii wananchi nao wakakubaliana na mikakati hii na kuamua kubadilika. Wanajamii wa Iringa wamesema watautumia vizuri mradi huo ili kuhakikisha kwamba si watu wachache tu wanafaidi na rasilimali zitokanazo na misitu na pia kuhakikisha wanahifadhi misitu kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye. Wananchi wamefurahia kupata mafunzo ambayo yatawasaidia wao kufuatilia utawala katika misitu na kupima kiwango cha uwazi katika mgawanyo

wa rasilimali zitokazo msituni ikijumuisha mapato na matatumizi ya fedha. Pamoja na kuupokea mradi huu wa haki katika misitu, wanajamii wa Iringa wameelezea changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika suala zima la uhifadhi wa misitu.

Changamoto kubwa ni ukosefu wa vitendea kazi mfano mabuti, sare za askari doria, usafiri wa kufika eneo la uharibifu mfano baiskeli, silaha kama mapanga. Wanajamii hao wameomba wapatiwe vifaa hivi kupitia mradi huu na hivyo kazi ya ulinzi itakuwa rahisi kwao ukilinganisha na hali ilivyo sasa kwa kuwa hakuna marefu yasiyo na ncha na kila atakayeamua kuchuma janga, basi atakula na wakwao. Pia kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu mazingira kwa ujumla, wanajamii hao wameomba wapate elimu hiyo kupitia mradi wa haki katika misitu, kweli elimu ni kama bahari, haina mwisho na matumizi yake ni popote. Matatizo mengine ni kama, kukosekana kwa ulinzi shirikishi na ushirikishwaji wa jamii katika masuala yahasuyo misitu, kukosekana kwa uaminifu kwa baadhi ya viongozi wa serikali katika matumizi ya rasilimali za misitu, kukosekana kwa ziara za mafunzo kwenye maeneo yaliyofanikiwa zaidi, kutopimwa kwa baadhi ya misitu yao na mambo mengineyo yahasuyo uhifadhi wa misitu. Hoja zote



Wanamtandao wa Idete wakipata mafunzo kwa ajili ya ufuatiliaji wa utawala bora katika sekta ya misitu

zilizibiwa na mratibu wa kanda nyanda za juu kusini Bwana Remmy Lema na kuwapa tumaini jipya wanajamii hao kuwa ofisi zimesogea maeneo walipo na suala la ufuatiliaji na ukaribu kwa wanajamii litakuwa sio tatizo tena bali watumie vizuri fursa hii adimu kutoa taarifa za uharibifu wa misitu ili hatua za makusudi zichukuliwe kwa haraka zaidi tofauti na kipindi cha nyuma. Pia matumizi mazuri ya mafunzo yaliyotolewa ili kupima mambo mbalimbali katika misitu mfano utawala bora. Ama kweli kimfaacho mtu chake.



Wanamtandao wa Kitapilimwa wakiimba wimbo kwa shangwe baada ya kuwapelekea mradi wa haki katika misitu.

